

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baiskeli Dar es Salaam  
Tarehe `23 Juni 2007.**

**Waliohudhuria**

Abdalha Joseph  
Ally Saidi Mohamedi  
Ally Salum  
Bakari Sadiki  
Elaine Baker  
Filbert Mbecha  
Hemedi Juma  
Izdoly Aludo Kihalule  
Juma Ali Salehe Jongo  
Jumanne Idd Selemani  
Kibwana Mohammad Msiga  
Kilenja Kasim Ramadhan  
Mejah Mbuya  
Mrisho Rumuli  
Paulo Atibu  
Prosper Nyaki  
Ramadhani Rajabu Nyengo  
Rashidi Saidi Karanji  
Rematus Nghazambi  
Suddi Saidi

**Wanachama Wapya**

Kulikuwa na wanachama wageni 7 na walikaribishwa na kujitambulisha.

**Mawasiliano na manispaa ya Ilala**

Prosper aliarifu kuwa amealikwa kuhudhuria mkutano wa kikosi cha kwanza cha nguvu kazi katika manispaa ya Ilala kuhusu msongamano barabarani uliofanywa tarehe 21 Juni Alhamisi. Katika mkutano huu iliamuliwa kuwa Maguta (baiskeli za tairi tatu zibebazo mizigo) zitatakiwa kusajiliwa katika kata zao na kutakuwa na maeneo maalum ya kusubiri abiria / wateja. Sheria moja itatumika pia kwa pick- up na taksi. Watatakiwa kulipa ada ya usajili au kodi. Hii ilionekana kukubalika kwa wanachama kwani ada na kodi zilikuwa nzuri na kwamba waliruhusiwa kuhudumia maeneo yote ya jiji ila tu maeneo ya kusubiria yalizuiwa. Ilionekana pia kuwa ni njia nzuri kwani itakuwa rahisi kupatana bei na mteja kwa kilo.

Hata hivyo ilikazwa kuwa lugha itakayotumika kwa mawasiliano kuhusu sera ni muhimu. Ikiwa lugha kama “kuondoa au kupiga marufuku” itatumika itakaririwa vibaya na waandishi wa habari na polisi na kusababisha maguta kugombana Manispaa ya Ilala inatakiwa kutoa nyaraka za sera zao kwa usahihi bila utata.

Prosper alitaarifu kuwa masuala ya uwepo wa barabara kwa wapanda baiskeli na maguta yalijadiliwa.

Mkazo uliwekwa pia, kuwa Ilala Manispaa iwasiliane kikamilifu na UWABA kujulisha kuhusu mikutano yote na mabadiliko yoyote ya sera. Nyongeza, kuamua sera katika mikutano isingekuwa na maana bila mawasiliano yanayoeleweka kwa sera ya nchi na utekelezaji.

Tulimshukuru prosper kwa mawasiliano na maelezo kuwa UWABA itaweza kuendelea kuwa mwakilishi mzuri wa wapanda baiskeli kwenye mkutano wa nguvu kazi

### **Msafara wa baiskeli**

Elaine aliarifu kuwa amechapa barua kuomba ufadhili kama ilivyoandaliwa kwenye mkutano uliopita. Juma alitumia siku mbili kusambaza barua hizo. Zilitumiwa kwenye ubalozi wa uholanzi, kampuni ya Mohammad, Knight Support, Kampuni ya kutengeneza Maguta na ZANTEL. Jumatatu atapeleka barua Bakresa. Juma alichukua namba za simu za kila ofisi.

Elaine alisema atafuatilia kwa simu wiki ijayo na kujaribu kuwasiliana na meneja masoko. Mejah alisema itakuwa muhimu kutuma barua ya kualika Knight Support na shule ili kupata idadi kubwa ya wapanda baiskeli. Alipata pia maelezo toka kwenye kampuni ya china ya kuuza Icecream kwa baiskeli, Sinu – Tanzania Fuwano yenye makao makuu kiwalani.

Barabara zilizo kwenye mpango wa kujengwa

Juma alisambaza barua TANROAD Dar es Salaam, Ubungo na washauri wanne kati ya sita wa wajenzi wa barabara tatu – Sam Nujoma, Nelson Mandela na Kilwa. Atapeleka barua mbili zilizosalia jumatatu, pia alipata namba zao.

### **Sehemu ya Mkutano na ofisi ziliko**

Mkutano huu ulikuwa wa kwanza kwenye eneo jipya la mahakama ya Ndizi, Mabino. Mwamko wa mkutano ulikuwa mkubwa na wanachama wapya walijiunga. Jumanne alipanga na wenye baa kuhusu viti na soda.

Mkutano ulikubali kuwa ni vyema kuwa na ofisi eneo hili. Kuna chumba kitupu kidogo karibu na ofisi ya Jumanne anakotengenezea maguta. Hii ilionekana ni jema, na kwa vile Jumanne na Rashid wanafanaya kazi karibu wataweza kujibu maswali na kutoa maelezo kwa watu watakaofika hapo ofisini. Tutaweka maelezo, mabango n.k kuhusu UWABA na fomu za uanachama kwa watu kujiunga baada ya kuhamasishwa na UWABA.

Kodi ya ofisi itakuwa kati ya elfu 20 Na 30 Kwa mwezi Jumanne alipendekeza kwamba badala ya kuwa na gharama za kila siku ni bora kuwekeza kwenye guta. Hela itakayopatikana kwa kukodisha guta itatumika kwa kodi ya chumba cha ofisi. Guta linagharimu Tsh 330,000. Elaine alisema atachunguza ikiwa watu anaowafahamu wanaweza kuchangia gharama kiasi, na wanachama watachangia itakayobakia.

**Akaunti ya Benki**

Ilikubalika kufungua akaunti katika Benki ya NBC tawi la magomeni. Kikao kitafuatilia namna ya kufanya hii ni muhimu hasa ikiwa tupata ufadhili wa Msafara.

**Mengineyo**

Elaine aliarifu kuwa Shukuru (ambaye hakuwepo kwenye mkutano) Alihudhuria mkusanyiko wa serikali Mnazi Mmoja na kwenye banda wakala wa Barabara TANROAD aliibua hoja kuhusu wapanda baiskeli na maafisa waliokuwepo na alipewa kipeperushi cha TANROAD

Elaine alichukua picha za watu/ wanachama ambao hawajapata vitambulisho ili vitengenezwe.

Mejah alishauri tuongee na askari wa usalama barabarani ili watoe elimu kuhusu haki na wajibu wa wapanda baiskeli barabarani